TANGAZO LA SERIKALI NA. 376 la tarehe 26/5/2023

SHERIA YA UWAKALA WA MELI TANZANIA,
SURA 415

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 28(3))*

TOZO ZA UWAKALA WA MELI, 2023

## SEHEMU YA KWANZA
## VIFUNGU VYA AWALI

Jina na kuanzakutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Tozo za Uwakala wa Meli ya mwaka, 2023 na itaanza kutumika siku kumi na nne kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Amri hii itatumika kwa mawakala wa meli waliopewa leseni kwa mujibu wa Sheria.

Tafsiri

Sura 415

3. Katika Amri hii, isipokuwa kama muktadha unahitaji vinginevyo:

"hati ya kukabidhi mzigo" maana yake ni nyaraka inayotolewa na wakala wa meli kwa niaba ya msafirishaji majini, kwenda kwa muhusika aliyetajwa ikimruhusu mwendesha bandari au bandari kavu kukabidhi mzigo kama ilivyoainishwa katika hati ya mizigo majini kwenda mtu aliyetajwa;

"hati ya mzigo majini" maana yake ni nyaraka inayotolewa na msafirishaji majini, au wakala wake au nahodha wa meli kwa niaba ya msafirishaji, kwenda kwa mtumaji mzigo kama mkataba wa kubeba bidhaa zilizoainishwa na inathibitisha kupokea mzigo melini kwa ajili ya kusafirishwa na msafirishaji na inathibitisha umiliki wa bidhaa kwa mtu atakayewasilisha, katika kituo kilichoainishwa, kwa msafirishaji

au wakala wake;

"mpokeaji mzigo" maana yake ni mtu ambaye anatumiwa mzigo uliopokelewa kubebwa kwenye meli na ambaye ametajwa hivyo kwenye hati ya mzigo majini;

"mtumaji" maana yake ni mtumaji mzigo aliyetajwa katika hati ya mzigo majini ambaye anawajibika kuanzisha mchakato wa kusafirisha, na ambaye anawajibika kulipia gharama za usafirishaji au kuingia mkataba na msafirishaji kuhusu namna gharama za usafirishaji zitakavyolipwa;

"tozo" maana yake ni gharama au bei pamoja na vigezo na masharti yanayotumiwa na mtoa huduma anayedhibitiwa;

Sura 415

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania;

"Shirika" maana yake ni Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania lilioanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria; na

"wakala wa meli" maana yake ni kampuni iliyopewa leseni ya kutoa huduma za uwakala wa meli katika bandari za bahari kwa mujibu wa Sheria.

## SEHEMU YA PILI
## TOZO

Tozo zilizoidhinishwa

4. Tozo za uwakala wa meli zilizoidhinishwa zitakuwa ni zifuatazo:

(a) tozo ya kukabidhi mzigo;
(b) tozo ya utoaji hati ya mzigo majini;
(c) tozo ya mabadiliko; na
(d) tozo nyinginezo kama zitakavyoelekezwa katika amri nyingine za kiudhibiti.

Viwango vya juu vya tozo

5. Viwango vya juu vya tozo zilizoidhinishwa za uwakala wa meli vitakuwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali.

## SEHEMU YA TATU
## VIFUNGU VYA JUMLA

Uunganishaji mifumo

6. Wakala wa meli atatakiwa kufanya yafuatayo:

(a) kutumia mifumo sahihi ya TEHAMA kuwezesha utoaji wa hati za kielekroniki za makabidhiano ya mizigo ili kulinda mzigo na kuongeza ufanisi katika hatua za makabidhiano; na

(b) kuunganisha mfumo wake wa TEHAMA na mfumo wa TEHAMA wa pamoja na inapolazimu kuunganisha mfumo wake na mifumo ya bandari na bandari kavu ili kuwezesha utumaji kielektroniki wa hati za kukabidhi mzigo.

Kuisha kwa muda wa matumizi ya hati ya kukabidhi mzigo

7. Shirika litatangaza muda wa chini wa kuisha kwa matumizi ya hati ya kukabidhi mzigo iliyotolewa na wakala wa meli kwa mpokeaji wa mzigo ili kuongeza ufanisi na kuulinda mzigo ulio katika hatua za makabidhiano.

Ufutaji wa Amri SMTRA/01/2010 na TASAC/01/2019

8. Amri za Tozo Na. SMTRA/01/2010 na TASAC/01/2019 kuhusu tozo za mawakala wa meli zimefutwa.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya 5)*

VIWANGO VYA JUU VYA TOZO VILIVYOIDHINISHWA

| Tozo | Inatozwa kwa | Kiwango cha Juu |
|---|---|---|
| Tozo ya Kukabidhi Mzigo | Hati ya Mzigo Majini | USD 15 (bila VAT) |
| Tozo ya Utoaji Hati ya Mzigo Majini | Hati ya Mzigo Majini | USD 38.14 (bila VAT) |
| Tozo ya Mabadiliko | Ombi | USD 59.32 (bila VAT) |

Dar es salaam,
25 Aprili, 2023

KAIMU ABDI MKEYENGE,
*Mkurugenzi Mkuu*